

**OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA IRINGA**



Barua zote ziadikwe kwa:
Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya
Simu nambari: +255 (026)- 2702585/2702828
Nukushi, +255(026)-2701776/2700580/270175

S.L.P. 108,
IRINGA.
TANZANIA

Barua pepe: ded@iringadc.go.tz
Tovuti: www.iringadc.go.tz

TAARIFA KWA UMMA

**HALMASHAURI YA WILAYA YA IRINGA IMESAINI MIKATABA MIWILI YA
MAENDELEO YENYE THAMANI YA TSHS. BILIONI 4.8**

Halmashauri ya Wilaya ya Iringa leo tarehe 16/04/2018 imesaini Mikataba 2 ya Upanuzi wa Miradi ya Maji yenye thamani ya Tshs. Bilioni 4.8.

Mikataba hiyo ni;

1. Upanuzi wa Mradi wa Maji Pawaga kwenda vijiji vine vya Kata ya Mlinge, kujenga mabomba ya kusambaza maji kwenda Magombwe, Isele, Kinyika na Kisanga chini ya Mkandarasi GNMS Contractors LTD wa S.L.P 107 Iringa, kazi hii itagharimu shilingi bilioni 3,216,845,931 na itatekelezwa kwa muda wa miezi 18.
2. Upanuzi wa Mradi wa Maji Pawaga kwenda vijiji vine vya Kata ya Mlinge, Ujenzi njia kuu mpya ya usambazaji 14.6km kutoka tanki la maji masafi kwenda kwenye tanki la Luganga na Magozi, kutengeneza kituo cha kusafirishia maji, tanki Ilolompya 50m³, Kimande 75m³ na Mbuyuni, chini ya Mkandarasi M/S HEMATEC INVESTMENT LTD wa S.L.P 34078 Dar-es-salaam, kazi hii itagharimu shilingi bilioni 1,647,262,810 na itatekelezwa kwa muda wa miezi 12.

Upanuzi wa Miradi hii ya maji ikikamilika inakusudiwa kuwahudumia wananchi zaidi ya 20,000 wa vijiji vya Magombwe, Isele, Kinyika na Kisanga, pia kukamilika kwa Miradi hii kutawapunguzia wananchi adha ya kufuata maji umbali mrefu na kupunguza magonjwa yatokanayo na ukosefu wa maji.

Mikataba hii imesainiwa na Mwanasheria wa Halmashauri Bi. Kissah Mbilla pamoja na Mwenyekiti wa Halmashauri Mh. Stephen Mhapa, Mkurugenzi wa Halmashauri Bw. Robert Masunya na Wakandarasi wa Miradi hiyo miwili.

Imetolewa na

Ofisi ya Habari na Uhusiano

Halmashauri (w) Iringa

